

**Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Rais  
na Wabunge, 1985**

## **TAARIFA YA UCHAGUZI MKUU WA RAIS NA WABUNGE, 1985**

### **Utangulizi:**

Katika Tanzania Uchaguzi wa Rais na Wabunge hufanywa kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Katiba. Kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1985 Katiba inayohusika ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 1984.

Mbali na Katiba, uchaguzi pia huendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Uchaguzi na kanuni/maadili yaliyowekwa na Chama kwa mujibu wa sheria hizo. Kwa kuzingatia haya yote taarifa hii inakusüdia kutoa sura ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1985 katika mambo makuu yahuusyo Aina za Wabunge; Majimbo ya Uchaguzi; Maandalizi ya Awali, Fedha, Vifaa, Watendaji; na Ratiba ya Uchaguzi.

### **Aina ya Wabunge:**

Katika Mkuutano wake wa mwezi Oktoba, 1984 Bunge lilipitisha Mu swada wa Sheria ya Mabadiliko ya Nne katika Katiba ya Nchi, ya mwaka 1984. Kwa kadiri sura ya Bunge inavyohusika Muswada huo uliletia mabadiliko makubwa yafuatayo:

- (a) Kupunguzwa kwa idadi ya Wabunge wa kuteuliwa.
- (b) Kuanzishwa kwa nafasi maalum za wanawake Bungeni.
- (c) Kufutwa kwa Wabunge wanaowakilisha Mikoa.
- (d) Kurejeshwa kwa utaratibu wa kuwa na Wabunge zaidi ya mmoja katika baadhi ya Wilaya.
- (e) Kuongeza idadi ya Wabunge wa kuchaguliwa na wananchi.

Kwa jumla basi, kwa mujibu wa fungu la 66 la Katiba, kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 15 ya mwaka 1984 aina zote za Wabunge ni kama ifuatavyo:—

### **1. Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha Wilaya za Uchaguzi za Mbunge mmoja:**

Katika uchaguzi wa mwaka 1985 Wilaya hizo zilikuwa 85 na zote ni za Tanzania Bara.

**2. Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha Wilaya za Uchaguzi za Wabunge wengi:**

Katika uchaguzi wa mwaka 1985 wilaya hizo ziliwa 27 na zikawa na jumla ya Wabunge 84. Katika wilaya hizo, kumi ni za Tanzania Zanzibar na zina jumla ya Wabunge 50, na wilaya nyingine 17 (zenye Wabunge 34) ni za Tanzania Bara.

**3. Wabunge Wanawake kumi na watano waliochaguliwa na Bunge kutoka mionganoni mwa watu waliopendekezwa na Jumuia ya Wanawake wa Tanzania mionganoni mwao angalao Watano Wakiwa Wanatoka Tanzania Bara na Watano Wakiwa Wanatoka Tanzania Zanzibar.**

Orodha ya majina ya waliopigiwa kura kwa mujibu wa kifungu hiki ipo katika Nyongeza "F".

**4. Wabunge Watano Waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi Kutoka Mionganoni mwa Wajumbe Wake:**  
(Tazama majina yao katika Nyongeza "G".)

**5. Wabunge wa Taifa Kumi na Watano waliochaguliwa na Bunge kutoka Mionganoni mwa majina ya Wagombea Uchaguzi wa Wabunge Yaliyopendekezwa na Jumuia za Wananchi Zinazoongozwa na Chama:**

(Tazama Nyongeza "E").

**6. Wabunge Kumi na Watano Waliochaguliwa na Rais, Mionganoni mwao Angalau Watano Wakiwa Wanatoka Tanzania Bara na Watano Wakiwa Wanatoka Tanzania Zanzibar;**  
(Tazama Nyongeza "H").

**7. Wakuu wa Mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano ambao Watakuwa Wabunge kwa mujibu wa Madaraka Yao:**

Kulingana na idadi ya sasa ya mikoa jumla ya watu walioingia Bungeni kwa mujibu wa kifungu hiki ni 25.

Jumla ya Wabunge wote ni 244.

**Maandalizi ya Awali:**

Sehemu kubwa ya maandalizi hayo ya awali ilihu upatikanaji wa takwimu za wapiga kura na za vifaa. Katika ukusanyaji wa takwimu za wapiga kura tulizingatia takwimu za idadi ya watu kama zilivyokusanywa katika sensa ya mwaka 1978; pia tulizingatia hesabu za namna hiyo kama zilivyoletwa kwetu na Maafisa Tawala wa Wilaya mbali mbali. Aidha katika takwimu zinazohusu vifaa tulizingatia pia kumbukumbu zilizokuwepo katika ofisi ya Tume ya Uchaguzi, na kumbukumbu zilizoletwa na Maafisa Tawala wa

Wilaya. Pia maafisa wa Tume walifanya ziarà katika baadhi ya wilaya kwa madhumuni ya kukagua hali halisi ya vifaa vya uchaguzi pamoja na kujifunza kutoka kwa wenzetu wanaohusika na utekelezaji wa shughuli za uchaguzi huko wilayani.

Kwa kuzingatia idadi ya watu kutokana na sensa ya mwaka 1978 (ikiwa ni pamoja na kuzingatia viwango vya vifo na ongezeko la watu); kwa kuzingatia takwimu zilizopatikana kutoka wilayani; na kwa kuzingatia idadi halisi ya watu waliojiandikisha katika uchaguzi Mkuu wa Rais/Wabunge wa mwaka 1980 (na pia katika uchaguzi wa madiwani wa mwaka 1984) Tume ilikadiria kwamba katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1985 kiasi cha watu milioni 9.1 kingejiandikisha kama wapiga kura. Hivyo kwa tahadhari vifaa vilivyotayarisha vilikuwa ni vya kutosheleza mahitaji ya wapiga kura milioni kumi.

Kwa bahati mbaya inasikitisha kuserna kwamba kiasi hiki hakikuweza kufikiwa; idadi halisi ya waliojiandikisha ilikuwa 6,901,555 (asilimia 56 tu ya walioskadirwa).

Yapo matatizo kadhaa ambayo yalijitokeza wakati wa maandalizi hayo ya awali. Baadhi yake ni haya yafuatayo:

(a) *Baadhi ya Maafisa Tawala wa Wilaya kuleta Makisio ya Juu Mno Kuhusu Idadi ya Wapiga Kura:*

Hali hii inaweza kuwa imesababishwa na mambo mengi yakiwemo:

- (i) Kutofanya hesabu halisi na kubuni tu hesabu hizo kutoka ofisini kutokana na matatizo ya usafiri.
- (ii) Baadhi ya Maafisa Tawala kutojihusisha na mambo ya uchaguzi tangu mapema na kuifanya kazi hiyo paparapapara siku zinapomalizika.
- (iii) Kutokuwepo na kumbukumbu za kudumu zinazoaminika kuhusu hali ya idadi ya watu katika ofisi za Maafisa Tawala.

(b) *Maafisa Tawala wa Wilaya (Baadhi Yao) Kutoleta Kabisa takwimu za Makadirio ya Wapiga Kura:*

Kwa sababu zisizoelewka baadhi ya Maafisa Tawala wa Wilaya hawakuleta kabisa takwimu zozote kuhusu makadirio ya wapiga kura, licha ya kukumbushwa mara kadha wao wenyewe au kupitia ngazi za juu za utawala. Hali hiyo ililetä matatizo makubwa katika ukadiriaji wa vifaa vilivyohitajika. Ufumbuzi uliofanyika ni kuongeza tu asilimia 25 juu ya idadi ya wapiga kura wa mwaka 1980.

(c) *Hifadhi Mbaya ya Vifaa na Kutoa Idadi ya Vifaa Bila Kuvikagua:*  
Katika Wilaya nyingi tulizotembelea tumeona kwamba vifaa vya uchaguzi havitunzwi kwa namna inayofaa—hasa masanduku ya kura. Katika sehemu nyingi vifaa hivyo vimetupwa tu hapa na pale uwani (ambako vinanyeshewa mvua na kuchakazwa na juu) au vimelundikwa na vikorokoro vingine kiasi kwamba ni vigumu kujuu vipo vingapi.

Aidha baadhi ya wahusika wilayani walituletea takwimu zinazoonyesha idadi ya vifaa walivyonyavyo bila kuvikagua vifaa hivyo na kuhakikisha kwamba kweli vipo na ni vizima. Matokeo yake ni kwamba siku ya uchaguzi inapokaribia inagundulika kwamba vifaa hivo havitoshi kwa sababu ya upungufu au ubovu wa baadhi ya vifaa.

Tungependa kusisitiza **kwa niguvu sana kwamba:**

- (a) Ni muhimu sana kanuni za utunzaji wa vifaa vya Serikali na uhakikimali zizingatiwe kwa vifaa vya uchaguzi pia.
- (b) Wakati wote ziwepo kumbukumbu za kuaminika katika ofisi za Wasimamizi wa Uchaguzi zinazoonyesha idadi na halisi ya vifaa vya uchaguzi.

Hitilafu hiyo baina ya takwimu tulizoletewa na idadi halisi ya vifaa vilivyopo wilayani iligunduliwa na Maafisa wa Tume katika sehemu kadhaa walizotembelea mnino Agosti na Septemba, 1984. Hivyo hatua zilichukuliwa mapema kuleta Dar es Salaam vifaa muhimu kama vile kufuli na mihuri. Ni wazi kwamba hatua hiyo iliongeza gharama za uchaguzi lakini walau ilitu hakikishia kuwapo kwa kiasi chote cha vifaa ambavyo tulivihitaji kwa wakati tulipovihitaji. Kama hatua hiyo hainge chukuliwa ulikuwepo uwezekano wa kujikuta, katika dakika za mwisho, kwamba kuna upungufu wa vifaa kadhaa, na hatua yoyote ya kutengeneza vifaa hivyo wakati huo ingeigharimu Serikali fedha nyingi zaidi.

Kwa ajili hii, baada ya uchaguzi wa mwaka 1985 tumeagiza kufuli zote zirejeshwe Dar es Salaam. Sehemu kubwa ya kufuli hizo imekwisha kurejeshwa, na yamkini, tutaitisha pia kuletwa kwa mihuri ya aina zote.

#### **Fedha:**

Shughuli nyingi za uchaguzi zimetendeka katika miaka ya fedha ya 1984/85 na 1985/86. Katika mwaka wa fedha 1984/85 Hazina iliidhinisha matumizi ya Sh. 32,052,500/-, hasa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali. Katika jumla hiyo kulikuwepo pia kiasi cha Sh. 15,646,300/- kwa ajili ya ununuzi wa karatasi mbali mbali na mitambo mipya ya kuiwezesha Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali kumudu kazi za uchaguzi kwa ufanisi.

Aidha katika mwaka wa fedha 1985/86 Hazina iliidhinisha matumizi ya Sh. 150,894,400/- sehemu kubwa ya fedha hiyo ikiwa ni kwa ajili ya gharama za uendeshaji kama vile semina kwa watendaji mbali mbali, posho, petroli n.k. Hivyo ukijumlisha kiasi hiki na kile kilichotolewa katika mwaka 1984 utaona kwamba kwa jumla kiasi kilichokuwa kimeidhinishwa kwa shughuli zote za uchaguzi ni Sh. 182,946,900/-.

Katika suala hili la fedha za uchaguzi yapo pia matatizo kadhaa ambayo yalijitokeza, yakiwemo haya yafuatayo:

(a) *Fedha za Uchaguzi Kutotolewa mapema na Hazina:*

Maombi ya awali ya fedha za uchaguzi kwa mwaka 1984/85 yaliwasilishwa HAZINA mapema na majadiliano ya kwanza baina ya HAZINA na Bunge yalifanyika tarehe 10 Mei, 1984. Lakini licha ya jithihadu kadhaa zilizofanywa idhini ya kutumia Sh. 32,052,500/- ilitolewa tarehe 29 Desemba, 1984; hata hivyo fedha hizo, hazikuweza kupatikana mpaka tarehe 12 Machi, 1985.

Tunapenda kusisitiza kwamba shughuli za uchaguzi zina ratiba maalum iliowekwa Kikatiba na au Kisheria. Kama jambo fulani halikutendeka katika siku iliyopangwa litendeke, Katiba/ Sheria itakuwa imevunjwa, na matokeo yake yanaweza kuwa mabaya siyo tu kiuchumi bali hata kisiasa. Ni matumaini yetu kwamba kwa siku zijazo. Wizara ya Fedha, Mipango na Uchumi itayafikiria maombi ya fedha za uchaguzi na kuyapa umuhimu unaostahili.

Aidha katika mwaka 1985, kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha za kigeni kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kukimu Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali; na kutokana na kuchelewa mno kutolewa kwa "Letters of Credit" kwa ununuzi wa mitambo hiyo, hata baada ya kupatikana kwa kibali cha Hazina/Benki Kuu, athari zifuatazo zimekuwepo:

- (i) Mitambo hiyo imechelewa kufika, hivyo haikushughulikia kazi za uchaguzi.
- (ii) Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali imeshindwa kumudu shughuli za uchaguzi kutokana na kukosekana kwa mitambo hiyo.
- (iii) Kazi fulani fulani za uchaguzi imebidi zichapishwe na Mashirika/Makampuni binafsi (KIUTA, PRINTPACK; ELIMU; na TANZAM International Marketing)—Jumla ya Sh. 3,120,345/- zimetumika kuyalipa Mashirika/makampuni haya. Siyo tu kwamba fedha hizo hazikuwemo katika Makadirio ya shughuli za uchaguzi; lakini pia kitendo cha kusambaza hapa na pale uchapishaji wa nyaraka nyeti kama

zá uchaguzi si kitendo kizuri kiusalama, hasa kinapofanywa katika dakika za mwisho ili tu kuokoa jahazi linalotaka kuzama.

- (iv) Uchapishaji wa karatasi za kura bubu haukuweza kukamilishwa na katika sehemu nyingi hapa nchini karatasi hizo hazikuweza kufikishwa.

Tunafikiri kwamba moja ya sababu za ucheleweshaji hiu katika utoaji wa fedha za uchaguzi inatokana na kiasi kikubwa mno cha fedha ambazo katika mwaka wa Uchaguzi Taifa lilipaswa kubeba. Pengine mzigo huu ungalisambazwa katika kipindi cha miaka mitatu inayotangulia Uchaguzi Mkuu, huenda mzigo huu ungekuwa mwepesi kidogo kubebeka na uwezekano wa kuwepo ajizi katika utoaji wa fedha bila shaka ungepunguka sana.

Kwa sababu hizo zote tunashauri kwamba kwanza sehemu ya uchaguzi ya Ofisi ya Bunge iimarishwe ili shughuli za uchaguzi ziwe za kudumu; na pili serikali ifanye kila jitihada kutoa fedha za uchaguzi zinazohitajika katika mwaka fulani wa fedha kwa wakati zinapohitajika.

*(b) Kutotengwa Fedha za Kugharamia shughuli fulani za Chama zinazohusu Uchaguzi:*

Katika mambo ya Uchaguzi Chama kina majukumu mbali mbali. Lakini kwa mazoea Chama huwa hakitengi mapema (wala kupatiwa) fedha za kugharamia majukumu hayo. Aidha shughuli za Chama ambazo hugharamiwa moja kwa moja na Tume ya Uchaguzi ni chache sana.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1985 malalamiko mengi yametokea mionganini mwa watumishi mbalimbali wa Chama walioshughulikia uchaguzi kwa namna moja au nyiningine. Viongozi hao walijikuta hawamjui ni nani wa kuwagharamia kati ya Chama na Tume ya Uchaguzi.

Tunafikiri kwamba ipo haja kubwa kwa Chama kujiandaa kifedha ili kugharamia shughuli zake zinazohusu Uchaguzi, au Serikali ikubali kugharamia pia shughuli zote za Chama kiuchaguzi kwa kutoa fungu maalumu kwa Chama kwa shughuli za Uchaguzi.

**Vifaa:**

Vifaa muhimu vilivyonunuliwa, ni kama ifuatavyo:

- : Karatasi mbali mbali;
- : Mihuri;
- : Kufuli, na
- : Masanduku.

Tatizo kubwa lililojitokeza linahusu hasa ukosefu wa magari Wilayani. Hali hiyo iliwafanya Wasimamizi wa Uchaguzi waazime magari kutoka kwenye Idara za Serikali, Mashirika ya Umma, Vijiji na hata kwa watu binafsi. Tatizo lililopo ni kwamba magari hayo yanapoharibika wakati wa shughuli za Uchaguzi yalirejeshwa kwa wenyeve yakatengenezwe kwa vile Wasimamizi wa Uchaguzi hawakuwa na fungu lo lote la utengenezaji wa magari wa aina yo yote.

Tunaamini kwamba hali hii hairidhishi kwa jumla. Tunapendekeza kwamba Serikali ikubali kimsingi kwamba Mkurugenzi wa Uchaguzi awe na "discretion" ya kugaramia matengenezo madogo madogo ya magari yanayoharibika wakati yakiwa katika shughuli za Uchaguzi, na hivyo kuwe na kiasi maalum kitakachotengwa kwa ajili hiyo katika makadirio ya Uchaguzi.

#### **Watendaji:**

Kutokana na mfumo wa utawala ulioanzishwa na "Decentralization" ya mwaka 1972, Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ndio walioteuliwa kuwa Wasimamizi wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1975 na 1980. Baada ya kurejeshwa kwa Serikali za Mitaa mnamo mwaka 1982 vyeo hivyo vilifutwa na badala yake Wilayani vikaundwa vyeo vya Maafisa Tawala wa Wilaya (DAO) na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DED).

Katika uchaguzi wa 1985 Tume ilivateua Maafisa Tawala wa Wilaya kuwa ndio Wasimamizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriwa hivyo na Serikali. Lakini kama inavyofahamika Maafisa hao wana watumishi wachache mno na uhaba mkubwa wa vifaa (pamoja na magari); baadhi yao hawakuwa na uzoefu wa uendeshaji wa shughuli za uchaguzi; na kwa Wilaya fulani fulani hapakuwepo na ushirikiano unaostahili kati ya DAO na DED.

Tunashauri kwamba pengine suala la kuwaimarisha ma-DAO kwa kuwapatia watumishi/vifaa lingetazamwa; hali kadhalika uhusiano wao na ma-DED uchambuliwe kwa shabaya ya kuuimarisha.

#### **RATIBA YA UCHAGUZI:**

##### **1. Semina za Wasimamizi wa Uchaguzi:**

Semina za Wasimamizi wa Uchaguzi zilifanyika kuanzia tarehe 23 Aprili, 1985 hadi 25 Mei, 1985. Vituo vya Semina vilikuwa saba kwa nchi nzima (Mwanza, Unguja, Mtwara, Dodoma, Moshi, Mbeya na Morogoro); na katika kila kituo semina ilichukua siku mbili au tatu.

Waliohudhuria semina hizo ni Wasimamizi wa Uchaguzi (Maafisa Tawala wa Wilaya kwa vijijini na Wakurugenzi wa Miji/Manispaa kwa majimbo mengi ya mijini); Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (katika wadhifa wao kama Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi); Makatibu wa Chama wa Wilaya); Afisa mmoja kutoka kila ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi; na afisa mmoja pia kutoka kila Mkao. Semina hizo ziliendeshwa hasa na maafisa wa Bunge, lakini baadhi ya mada zilitolewa na Maafisa kutoka Hazina.

Mada zifuatazo ndizo zilizotolewa na kujadiliwa:

- (i) Lugha ya Uchaguzi na Mawasiliano.
- (ii) Kuandikisha Wapiga Kura.
- (iii) Kanuni za Ununuzi na Utunzaji wa Vifaa katika mazingira ya Uchaguzi.
- (iv) Uteuzi wa Mwanzo na wa mwisho.
- (v) Utaratibu wa Matumizi ya Fedha za Uchaguzi.
- (vi) Maandalizi ya Upigaji Kura na Utaratibu wake.
- (vii) Uteuzi wa Wasimamizi wa Vituo vya Kura.
- (viii) Utaratibu wa kuhesabu Kura.
- (ix) Malalamiko Dhidi ya Matokeo ya Uchaguzi.
- (x) Miiko ya Uchaguzi.

## 2. **Uandikishaji wa Wapiga Kura:**

Uamuza wa awali ulikuwa kwamba uandikishaji wa wapiga kura ufanyike kuanzia tarehe 24 Julai hadi 24 Agosti, 1985. Lakini baadae tarehe ya mwisho ilisogezwa mbele hadi 31 Agosti, 1985. Hiyo ilifanyika ili kufidia kipindi ambacho uandikishaji ulizorota kutokana na hekaheka za wananchi kubadili noti zao za zamani kwa noti mpya kwa mujibu wa agizo la Benki Kuu ya Tanzania.

Idadi halisi ya watu waliojiandikisha kwa nchi nzima ni 6,901,555. Ikilinganishwa na idadi ya watu waliojiandikisha katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1980 (6,969,803) idadi hii ya mwaka 1985 ni ndogo kwa watu 68,248. Idadi ya waliojiandikisha katika miaka ya 1980 na 1985 kwa kila jumbo la uchaguzi imo katika Nyongeza "A".

Kwa wale ambao wamehamia sehemu zingine baada ya uandikishaji kufungwa, Tume iliweka tarehe 15 Oktoba, 1985 kuwa siku ya mwisho ya kubadilishiwa kadi zao za kuandikishwa.

Ukiachia mbali suala la kubadilisha noti ambalo lilizorotesha uandikishaji, hapakuwa na matatizo mengine makubwa katika suala zima la uandikishaji. Ila ile hali ya usambazaji mbaya wa fomu namba moja, na kadi pia, liliendelea kujitokeza kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

### **3. Uteuzi wa Mwanzo:**

Siku ya Uteuzi wa Mwanzo kwa Wagombea Ubunge wa kuchaguliwa na wananchi ilikuwa tarehe 8 Agosti, 1985. Kwa wagombea Ubunge wa Taifa na Ubunge wa Kujaza Viti maalum nya Wanawake, tarehe ya mwisho ya kurudisha formu zao kwenye Jumuia zinazohusika ilikuwa tarehe 14 Agosti, 1985.

### **4. Mikutano ya Chama:**

Mikutano Mkuu wa Taifa kuteua jina la Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulifanyika tarehe 15 Agosti, 1985. Ndogu Ali Hassan Mwinyi ndiye aliyeteuliwa na Mikutano huo.

Mikutano Mikuu ya Wilaya ilifanyika nchini kote kati ya tarehe 21 na 31 Agosti, 1985 ili kutoa kura za maoni kwa wagombea ubunge wa kuchaguliwa na wananchi. Pia vikao nya Jumuia mbali mbali nya kupendekeza majina ya wagombea Ubunge wa Taifa, na wa viti maalum nya Wanawake; vilifanyika kati ya tarehe 19 na 31 Agosti, 1985. Kuhusu idadi ya kura za maoni kwa kila mgombea tazama nyongeza "B".

Halmashauri Kuu ya Taifa (N.E.C.) ya CCM ilikutana tarehe 11 Septemba, 1985 kwa ajili ya Uteuzi wa Mwisho wa Wagombea Ubunge wa kuchaguliwa na wananchi, wa Taifa, na wa Viti Maalumu nya Wanawake.

### **5. Kampeni za Uchaguzi:**

Mwanzoni ilipangwa kwamba katika Wilaya za Vijijini za Tanzania Bara kampeni zifanyike kuanzia tarehe 7 Oktoba, 1985 hadi 26 Oktoba, 1985; na katika Wilaya za Miji za Tanzania Bara na Wilaya zote za Tanzania Zanzibar, kuanzia tarehe 14 Oktoba, 1985 hadi 26 Oktoba, 1985. Lakini kutokana na tatizo la ukosefu wa mafuta (petroli) baadae iliamuliwa kwamba kampeni za uchaguzi nchini kote zifanyike kuanzia tarehe 14 hadi 26 Oktoba, 1985.

Wagombea Ubunge wa Taifa na wa Viti nya Wanawake walijieleza mbele ya Kamati ya CCM ya Wabunge tarehe 2 Novemba, 1985.

Kwa mara ya kwanza Waangalizi wa Uchaguzi waliohudhuria kampeni hizo walichaguliwa kutoka mikoa ya jirani kama ilivyopendekezwa katika taarifa ya Tume kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1980 (17:2). Lakini kutokana na viwango vidogo mno nya posho (Sh. 200/- au 250/-) vikilinganishwa na gharama halisi, Waangalizi wengi walikabiliwa na matatizo makubwa ya maisha huko walikopelekwa. Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waangalizi waliohusika kwa kufanya kazi yao vizuri hata katika hali ngumu iliyowakabili.

Lakini pamoja na moyo huo na shukrani hizo ni vyema ifahamike kwamba kazi ya Uangalizi wa Uchaguzi ni kazi inayobeba jukumu na mamlaka makubwa sana katika kulinda haki na demokrasi kwa jumla. Isitoshe, kazi ya uchaguzi ni kazi inayotokea mara moja kwa miaka mitano.

Kwa kuzingatia yote hayo tunapendekeza kwamba ipo haja kubwa ya kuongeza posho wanayolipwa Waangalizi wa Uchaguzi. Katika kuweka viwango hivyo isiwe lazime kulinganisha posho hizo na zile zinazotolewa kwa watumishi wa Serikali, au Chama.

#### 6. Siku ya Kupiga/Kuhesabu Kura:

Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, na wa Wabunge ulifanyika kote nchini Jumapili tarehe 27 Oktoba, 1985. Hakukuwa na matatizo makubwa isipokuwa huko Tarime ambako kituo kimoja (ROCHE) kiliathiriwa na matatizo ya uendeshaji na ikabidi wapige kura zao siku ya tarehe 28 Oktoba, 1985.

##### (a) Matokeo ya Uchaguzi wa Rais:

Matokeo ya uchaguzi wa Rais yalitangazwa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Chifu A. S. Mkwawa, tarehe 1 Novemba, 1985, kunako saa nne asubuhi kama ifuatavyo:—

"Ndugu Wananchi,

Kama wote minavyoju Uchaguzi Mkuu umefanyika pote nchini, Tanzania Bara na Visiwani, ili kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uchaguzi huo ulifanyika siku ya Jumapili tarehe 27 Oktoba, 1985.

Tume ya Uchaguzi imepokea idadi yote ya kura zilizopigwa kutoka katika kila jimbo la Uchaguzi Tanzania Bara na Visiwani. Matokeo yake ni kama ifuatavyo:—

1. Idadi ya Watanzania wote waliojiandikisha kupiga kura ni watu 6,901,555.
2. Kati ya hao waliojitekeza wakaenda kwenye vituo na wakapiga kura siku ya tarehe 27 Oktoba, 1985 ni 5,181,999. Idadi hii ni sawa na asilimia 74.98 ya Watanzania wote waliojiandikisha kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa 1985.
3. Katika kura hizo zilizopigwa idadi ya kura zilizoharibika ni 188,259 ambayo ni asilimia 3.64 ya kura zote zilizopigwa katika uchaguzi wa Rais wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.
4. Idadi ya kura za "Hapana" ni 215,626 ambayo ni sawasawa na asilimia 4.16 ya kura zote zilizopigwa katika Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano.

5. Idadi ya kura za "Ndiyo" ni 4,778,114 ambayo ni sawa na asilimia 92.20 ya kura zote zilizopigwa katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.
6. Kutohana na matokeo hayo, ndiyo kusema kuwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote waliojitekeza na kupiga kura zao wamemkubali mgombwea pekee wa Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
7. Hivyo basi kwa mujibu wa fungu la 41 Ibara ya 3 (a) ya Kätiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 15 ya mwaka 1984; sasa natangaza rasmi kuwa Ndugu Ali Hassan Mwinyi amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".

Matokeo kamili ya Uchaguzi wa Rais kwa kila jimbo (yakionyesha waliojiandikisha, waliopiga kura, Ndiyo, Hapana na zilizoharibika) yameonyeshwa katika Nyongeza "C".

- (b) Matokeo ya Kura za Wabunge kwa Majimbo yote ya Uchaguzi:  
Tazama Nyongeza "D".
- (c) Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge wa Taifa na wa Viti Maalumu vya Wanawake:  
Uchaguzi wa Wabunge wa aina hii ulifanyika Bungeni tarehe 2 Novemba, 1985. Matokeo ya Uchaguzi huo yameonyeshwa katika Nyongeza "E" (Taifa) na "F" (Wanawake).

#### **Malalamiko Mahakamani:**

Idadi ya malalamiko yaliyofikishwa mahakamani dhidi ya matokeo ya Uchaguzi ni 23. Malalamiko hayo yanahusu majimbo ya Uchaguzi ya Dimani; Mwera; Rufiji; Kisarawe; Temeke; Mtwara Mjini; Masasi; Mbeya Mjini; Mbozi; Kongwa; Singida Mjini; Singida Vijijini; Nzega; Shinyanga Mjini; Bukoba Mjini; Tarime; Arumeru; Kiteto; Moshi Vijijini; Rombo; Muheza; Pangani, Korogwe.

Mpaka wakati wa kutoa taarifa hii, Mahakama Kuu iliyokuwa ikisikiliza kesi hizi ilikuwa imeshabatilisha matokeo ya Uchaguzi katika Majimbo ya Kiteto na Singida Mjini, Singida Vijijini na Tarime.

#### **Shukurani:**

Shughuli za Uchaguzi ni nyngi na Washiriki wake ni wengi pia. Kuna vyombo vya kikatiba (kwa mfano Chama katika ngazi zake mbalimbali), kuna mashirika, idara na makampuni mbali mbali; kuna watendaji mbali mbali waliohusika kwa namna moja au nyngine, na hatimaye kuna wananchi wenywewe kwa jumla ambao shughuli nzima ya uchaguzi iliwigusa kwa namna moja au nyngine.

Ingawa haiwezekani kuwataja washiriki wote waliosaidia kufanikisha shughuli za uchaguzi, haiwezekani pia kushindwa kuwataja wasuatao:

1. Viongozi wa Chama katika ngazi zote.
2. Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Muungano; na pia wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.
3. Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasaidizi wao wote; Waangalizi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Vituo na Wasaidizi wao; Mawakili wa Upigaji Kura na Walinzi.
4. Mashirika yaliyokuwa mstari wa mbele katika suala la mawasiliano na usalirishaji wa vifaa, hasa Jeshi la Wananchi la Tanzania; Jeshi la Polisi; Shirika la Reli la Tanzania; Shirika la Posta/Simu la Tanzania; Shirika la Reli la Tanzania na Zambia; na Makampuni mengine ya mabasi/meli.
5. Idara ya Mpiga Chapa ya Serikali na wafanyakazi wake wote kwa jinsi walivyofanya kazi usiku na mchana, kukamilisha uchapishaji wa nyaraka na hati mbalimbali.
6. Mashirika/Makampuni ya KIUTA, PRINTPACK, Tanzania Internatiopnal Marketing, na Wizara ya Elimu, kwa mchango wao katika uchapishaji.
7. Katibu na Watumishi wengine wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa katika masuala mbali mbali.
8. Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge ambao tangu maandalizi ya Uchaguzi yalipoanza mpaka uchaguzi ulipokamilika hawakujua saa au sikukuu, na walifanya kazi yoyote iliyokuwepo bila kujali vyeo vyao au masilahi mengine.
9. Wananchi wote waliojitekeza kupiga kura na hivyo kuwakosoa kwa mara nyingine maadui wa demokrasi ya Chama Kimoja.

M. MWINDADI,  
*Mkurugenzi wa Uchaguzi*

### NYONGEZA

- "A"— Idadi ya Waliojiandikisha kupiga kura, 1980 na 1985, kwa Majimbo Yote ya Uchaguzi.
- "B"— Kura za Maoni zilizotolewa na Mikutano Mikuu ya Wilaya.
- "C"— Matokeo ya Uchaguzi wa Rais kwa kila Jimbo la Uchaguzi.
- "D"— Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge kwa Majimbo yote ya Uchaguzi.
- "E"— Uchaguzi wa Wabunge 15 wa Taifa (Jina, Jumuia iliyompendekeza, kura alizopata Bungeni, Wagombea waliochaguliwa).
- "F"— Uchaguzi wa Wabunge Wanawake,
- (i) Tanzania Bara.
  - (ii) Tanzania Zanzibar.
  - (iii) Mchanganyiko.
- "G"— Majina ya Wabunge Watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi.
- "H"— Majina ya Wabunge 15 walioteuliwa na Rais.

### NYONGEZA "A"

#### IDADI YA WALIOJIANDIKISHA KUPIGA KURA, 1980 NA 1985 KWA MAJIMBO YOTE YA UCHAGUZI

Jimbo la Uchaguzi	Lengo 1980	Waliojia- ndikisha 1980	Asilimia	Lengo 1985	Waliojia- ndikisha 1985	Asilimia
1. Amaan .....	72,462	47,712	65	6,680	5,447	81
2. Arumeru .....	92,730	88,392	95	111,530	94,562	84
3. Arusha .....	31,500	46,780	148	51,000	47,813	93
4. Babati .....	—	—	—	—	50,320	—
5. Bagamoyo .....	51,450	59,178	115	70,806	50,147	70
6. Bahi .....	—	—	—	168,154	67,295	40
7. Bariadi .....	99,725	98,959	99	139,790	116,776	83
8. Biharamulo .....	66,465	69,150	104	81,968	70,250	85
9. Bukoba Mjini .....	13,898	15,210	109	18,300	16,649	90
10. Bukoba Vijijini .....	265,764	100,043	37	137,550	98,700	71
11. Bukombe .....	—	—	—	—	48,743	—
12. Bumbwini .....	14,081	13,892	98	4,229	4,143	97
13. Buanda .....	68,267	—	—	92,108	63,637	69
14. Chaani .....	35,014	20,657	58	5,378	5,050	93
15. Chambani .....	—	—	—	5,513	4,373	79
16. Chilonwa .....	—	125,682	—	—	61,594	—
17. Chonga .....	23,817	19,046	79	4,900	3,959	80
18. Chunya .....	34,873	43,484	124	54,355	50,449	92
19. Chwaka .....	16,415	13,757	83	5,680	5,248	92
20. Dimani .....	20,612	16,766	81	7,962	5,293	66
21. Dodoma Mjini .....	83,820	75,010	89	90,012	65,523	72
22. Donge .....	—	—	—	5,510	5,285	95
23. Gando .....	23,538	23,201	98	10,656	4,515	42

NYONGEZA "A"—(naendelea)  
**IDADI YA WALIOJIANDIKISHA KUPIGA KURA, 1980 NA 1985 KWA  
 MAJIMBO YOTE YA UCHAGUZI**

Jimbo la Uchaguzi	Lengo 1980	Waliojia-ndikisha 1980	Asilimia	Lengo 1985	Waliojia-ndikisha 1985	Asilimia
24. Geita .....	162,045	117,855	72	150,000	119,995	79
25. Hai .....	81,611	64,697	79	69,599	57,118	82
26. Hanang .....	90,450	80,242	88	138,680	25,671	18
27. Handeni .....	90,186	70,002	77	93,689	64,111	68
28. Igunga .....	88,280	73,928	83	90,817	66,465	73
29. Ilala .....	144,033	134,413	93	161,295	111,682	69
30. Ileje .....	40,000	26,562	66	29,988	26,371	87
31. Iramba .....	93,754	90,571	96	108,685	92,506	85
32. Iringa Mashariki ...	146,433	127,925	87	159,906	67,279	42
33. Iringa Magharibi...						
34. Iringa Mjini .....	18,206	24,481	134	29,377	23,570	80
35. Jang'ombe .....	—	—	—	6,920	7,814	112
36. Kahama .....	93,500	105,252	112	177,634	89,240	50
37. Karagwe .....	—	—	—	70,000	59,612	85
38. Karatu .....	—	—	—	62,800	33,725	53
39. Kasulif .....	91,515	97,864	106	117,486	83,469	71
40. Kibaha .....	43,731	37,898	86	51,439	33,789	65
41. Kibondo .....	84,003	50,687	60	60,824	62,265	102
42. Kigoma Mjini .....	29,322	18,030	61	21,636	21,392	98
43. Kigoma Vijijini .....	101,961	62,921	61	75,505	65,279	86
44. Kikwajuni .....	—	—	—	4,788	3,545	74
45. Kilindi .....	—	—	—	6,100	5,482	89
46. Kilombero .....	69,628	62,395	89	77,353	58,187	76
47. Kilosa .....	116,223	105,357	90	127,418	109,649	86
48. Kilwa .....	54,836	42,110	76	50,539	39,345	77
49. Kinondoni .....	211,358	235,360	111	282,432	206,338	73
50. Kisarawe .....	94,442	65,515	69	78,618	55,944	71
51. Kishapu (Shinyanga V)	120,590	116,416	96	170,990	64,604	37
52. Kiteto .....	35,180	26,890	76	39,000	34,488	—
53. Kitope .....	—	—	—	5,135	5,234	101
54. Kiwani .....	—	—	—	—	4,649	—
55. Koani .....	—	—	—	5,589	5,945	106
56. Kojani .....	—	—	—	—	5,359	—
57. Konde .....	24,210	—	—	—	5,587	—
58. Kondoa .....	122,945	105,445	85	116,012	60,891	52
59. Kongwa .....	—	—	—	—	48,781	—
60. Korogwe .....	95,259	76,792	80	87,384	70,095	80
61. Kwahani .....	—	—	—	6,195	4,623	74
62. Kwamtipura .....	—	—	—	4,781	3,930	82
63. Kwimba .....	160,080	118,471	74	142,165	73,595	51
64. Kyela .....	54,710	48,705	89	61,088	43,833	71
65. Lindi Mjini .....	20,220	10,901	53	12,000	11,440	95
66. Liwale .....	22,394	19,063	85	23,828	17,160	72
67. Ludewa .....	26,610	28,904	108	31,668	26,473	83
68. Lushoto .....	99,881	95,888	96	115,065	74,697	64

NYONGEZA "A"—(inaendelea)  
 IDADI YA WALIOJIANDIKISHA KUPIGA KURA, 1980 NA 1985 KWA MAJIMBO  
 YOTE YA UCHAGUZI

Jimbo la Uchaguzi	Lengo 1980	Waliojia-ndikisha		Lengo 1985	Waliojia-ndikisha	
		1980	Asilimia		1985	Asilimia
69. Mafia .....	23,003	9,712	—	—	10,398	—
70. Magu .....	109,780	91,534	—	109,408	100,235	91
71. Magomeni .....	—	—	—	5,080	4,184	82
72. Mahenge .....	55,107	44,850	—	53,820	36,965	68
73. Makadara .....	—	—	—	3,119	2,603	83,45
74. Makete .....	45,000	36,734	81.63	43,881	37,325	85.05
75. Makunduchi .....	11,073	9,624	86.91	5,543	5,032	90.78
76. Malindi .....	—	—	—	4,735	3,448	72.81
77. Manyoni .....	62,319	47,230	75.78	56,676	42,473	74.94
78. Masasi .....	147,658	113,975	77.18	136,770	61,107	44.67
79. Maswa .....	104,975	118,288	112.68	148,750	65,345	43.92
80. Matemwe .....	—	—	—	—	5,163	—
81. Mbarali .....	—	—	—	—	44,911	—
82. Mbeya Mjini .....	30,000	39,748	132.49	47,797	40,276	84.44
83. Mbeya Vijijini .....	111,866	111,921	100.04	139,901	57,722	41.25
84. Mbinga .....	93,428	65,332	69.92	78,398	71,688	91.44
85. Mbozi .....	101,095	96,141	95.09	120,176	90,585	75.37
86. Mbulu .....	73,129	68,177	95.22	58,158	45,719	78.61
87. Meatu .....	—	—	—	—	45,991	—
88. Mfenesini .....	—	—	—	8,051	6,804	84.51
89. Mgogoni .....	—	—	—	—	5,496	—
90. Micheweni .....	15,940	19,066	119.61	—	6,295	—
91. Mikunguni .....	—	—	—	4,918	3,883	78.95
92. Misungwi .....	—	—	—	—	54,851	—
93. Mkanyageni .....	—	—	—	—	4,826	—
94. Mkinga .....	—	—	—	—	27,374	—
95. Mkoani .....	24,210	21,561	89.05	—	4,415	—
96. Mkunazini .....	—	—	—	5,163	3,663	70.94
97. Mkwajuni .....	—	—	—	—	5,570	—
98. Mlandege .....	—	—	—	5,790	4,083	70.51
99. Monduli .....	21,100	32,889	155.87	39,466	25,946	65.74
100. Morogoro Kaskazini	265,932	137,082	—	—	60,858	—
101. Morogoro Kusini ...	—	—	—	—	—	—
102. Morogoro Mjini .....	35,000	39,884	113.95	50,000	31,198	62.39
103. Moshi Mjini .....	26,366	35,951	136.35	39,480	31,564	79.94
104. Moshi Vijijini .....	144,000	100,543	69.82	168,120	94,756	56.36
105. Mpanda .....	45,372	33,304	73.40	39,964	32,440	81.17
106. Mpwapwa .....	123,573	107,979	87.38	134,450	60,330	44.87
107. Mtama .....	—	89,941	—	—	44,475	44,475
108. Mtambile .....	—	—	—	—	5,591	—
109. Mtambwe .....	—	—	—	—	5,255	—
110. Mtvara Mjini .....	22,800	24,408	107.05	31,702	20,161	63.59
111. Mtvara Vijijini .....	71,262	52,100	73.11	70,000	44,353	63.36
112. Musindu .....	96,178	67,885	70.58	115,240	76,700	66.66
113. Muheza .....	84,195	73,411	87.19	88,093	41,428	47.02
114. Muleba .....	38,060	77,083	202.53	98,500	68,823	69.65
115. Musoma Mjini .....	19,654	23,925	121.73	28,710	19,803	68.97

**NYÖNGEZA "A"—(inaendelea)**  
**IDADI YA WALIOJIANDIKISHA KUPIGA KURA, 1980 NA 1985 KWA MAJIMBO**  
**YOTE YA UCHAGUZI**

Jimbo la Uchaguzi	Lengo 1980	Waliojia-ndikisha 1980	Asilimia	Lengo 1985	Waliojia-ndikisha 1985	Asilimia
116. Musoma Vijijini ....	69,265	73,895	106.68	91,763	73,725	80.34
117. Muyuni .....	—	—	—	5,803	5,584	96.22
118. Mwanga .....	36,975	23,987	64.87	28,784	26,899	93.45
119. Mwanza .....	66,100	72,301	109.38	86,761	82,071	94.59
120. Mwembe— Makumbi .....	—	—	—	8,379	6,109	72.90
121. Mwera .....	—	—	—	7,865	5,389	68.51
122. Nachingwea .....	47,134	39,426	83.63	47,311	34,598	78.12
123. Namtumbo .....	—	—	—	43,634	30,572	70.06
124. Nanyumbu .....	—	—	—	—	37,514	—
125. Newala .....	307,188	129,321	42.09	76,300	46,825	61.36
126. Ngara .....	112,853	39,405	34.91	60,000	43,072	71.78
127. Ngorongoro .....	23,591	14,750	62.52	26,000	17,620	—
128. Njombe .....	97,146	97,146	100.00	104,665	93,832	89.64
129. Nkasi .....	46,656	30,986	66.41	38,733	32,929	85.01
130. Ntomoko .....	—	—	—	—	50,758	—
131. Nungwi .....	—	—	—	—	5,289	—
132. Nzega .....	113,390	91,462	80.66	109,754	91,209	83.10
133. Ole .....	—	—	—	—	5,335	—
134. Pandani .....	—	—	—	—	3,913	—
135. Pangani .....	20,601	12,466	60.51	15,750	10,710	68
136. Peramiko (Songea Mjini) .....	84,945	56,797	66.86	31,895	39,812	124.82
137. Rahaleo .....	—	—	—	5,423	4,194	77.33
138. Rombo .....	70,892	50,407	71.10	85,000	60,074	70.67
139. Rufiji .....	79,039	52,886	66.91	63,463	41,989	66.16
140. Rungwe .....	124,169	87,049	70.10	100,053	82,985	82.94
141. Rwanga .....	—	—	—	—	38,620	—
142. Same .....	28,800	37,628	130.65	43,582	34,345	78.80
143. Sengerema .....	99,921	93,542	93.61	68,093	91,499	134.37
144. Serengeti .....	31,110	29,601	95.14	43,700	35,692	81.67
145. Shinyanga Mjini .....	105,764	24,410	23.07	29,037	33,380	114.63
146. Singida Mjini .....	31,774	24,350	76.63	30,000	25,391	84.63
147. Singida Vijijini .....	116,000	96,032	82.78	147,052	98,551	67.01
148. Solwa .....	—	—	—	—	67,205	—
149. Songea Mjini .....	26,110	22,419	85.86	31,895	18,150	56.90
150. Sumbawanga Mjini .....	17,203	21,927	127.46	28,000	22,629	80.81
151. Sumbawanga Vijijini .....	56,797	65,460	115.25	78,552	61,765	78.59
152. Tabora Kaskazini ..	68,590	73,148	93.76	84,546	46,598	55.11
153. Tabora Kusini .....	30,000	—	—	46,277	31,600	—
154. Tabora Mjini .....	—	—	—	65,300	64,223	98.35
155. Tandahimba.....	70,144	57,799	82.40	60,120	58,996	98.13
156. Tanga' .....	83,377	86,164	103.34	103,396	95,382	92.24

NYONGEZA "A"—(inaendelea)  
**IDADI YA WALIOJIANDIKISHA KUPIGA KURA, 1980 NA 1985 KWA  
 MAJIMBO YOTE YA UCHAGUZI**

Jimbo la Uchaguzi	Waliojia-ndikisha Asilimia			Waliojia-ndikisha Asilimia		
	Lengo 1980	1980	1985	Lengo 1985	1985	Asilimia
158. Temeke .....	131,904	157,688	119.54	159,225	130,097	68.75
159. Tumbatu .....	—	—	—	—	5,289	—
160. Tumbe .....	—	—	—	—	4,607	—
161. Tunduru .....	70,330	58,458	83.11	66,604	51,379	77.14
162. Ukerewe .....	71,550	52,213	72.97	65,800	56,667	86.12
163. Urambo .....	50,000	47,260	94.52	65,979	54,649	32.82
164. Utaani .....	—	—	—	—	4,912	—
165. Uzini .....	—	—	—	6,719	5,753	85.62
166. Vitongoji .....	—	—	—	4,300	3,458	30.41
167. Wawi .....	—	—	—	3,356	3,805	113.37
168. Wingwi .....	—	—	—	—	3,618	—
169. Ziwani .....	—	—	—	5,600	4,632	32.71

**NYONGEZA "B"**  
**KURA ZA MAONI ZILIZOTOLEWA NA MIKUTANO MIKUU  
 YA CCM WILAYANI 1985**

**MKOA WA ARUSHA**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
1. Arusha		
	1. Ndugu A. O. Kinana .....	137
	2. Ndugu D. O. Mollel .....	1
	3. Ndugu G. Ole Marti .....	32
	4. Ndugu I. S. O. Kivuyo .....	2
	5. Ndugu I. A. Lembuya .....	34
	6. Ndugu Kipuyo Maganga A. Ole Titos .....	53
	7. Ndugu H. H. Mbaga .....	19
	8. Ndugu T. M. Msaky .....	34
	9. Ndugu E. A. Oning'o .....	2
	10. Ndugu W. N. Makenja .....	0
2. Arumeru		
	1. Ndugu Kirilo Japhet Ayo .....	213
	2. Ndugu Melikizedek Martin Ole Kisako .....	3
	3. Ndugu Emmanuel Abrahams Nanyaro .....	21
	4. Ndugu Samwel Lazaros Laizer .....	5
	5. Ndugu Peniel Ole Saitabau Lukumai .....	389
	6. Ndugu Valerian Langoi Kaaya .....	0
	7. Ndugu Bob Ndekirwa Eliahu Nasser .....	47
3. Babati		
	1. Ndugu Dodo Ahmed Amri .....	73
	2. Ndugu Qaresi Mateo Tluway Naasi .....	103

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
4. Hanang	1. Ndugu Murumbi Daniel Girengay ..... 2. Ndugu Sumaye Frederick Tluway ..... 3. Ndugu Gapchojiga Mefunya Gidamoni .. 4. Ndugu Qamara Laurent Baloho ..... 5. Ndugu Gitagno Donald Mateo Duncan ... 6. Ndugu Gwandu Stephen Ghubay Nakei .. 7. Ndugu Joseph Hussein Mkodo .....	60 336 46 41 10 7 8
5. Karatu	1. Ndugu George Baha Bura ..... 2. Ndugu Patrick Silverius ..... 3. Ndugu Simon Akonaay Iarmo .....	43 395 54
6. Kiteto	1. Ndugu Erasto Losioki ..... 2. Ndugu Habib Hassan Surumbu ..... 3. Ndugu Reuben Ole Kuney Kimaat..... 4. Ndugu George Matinda Ole Mbuki .. 5. Ndugu Ali Saidi Kipande .....	99 78 16 13 11
7. Mbulu	1. Ndugu Sulustian Akunaay Deeng'w ..... 2. Ndugu Mark Dagharo Maafa ..... 3. Ndugu Philip Sang'ka Marimo ..... 4. Ndugu Bartholomew Naftali Naman..... 5. Ndugu Joseph Surumbu Naman .....	81 45 257 30 3
8. Monduli	1. Ndugu Joseph Ole Muturu Lemomo ..... 2. Ndugu Orkurtuta Walina Kuukai .....	159 40
9. Ngorongoro	1. Ndugu Moringe Saiyalel Parkipuny ..... 2. Ndugu Tekan Michael Leitura Ole Konchellah .....	80 37

**MKOA WA IRINGA**

1. Ludewa	1. Ndugu Violet Mercy Baraka ..... 2. Ndugu Mathias Michael Kihale .. 3. Ndugu Mathayo Yohana Machoya .....	62 153 9
2. Iringa Mjini	1. Ndugu Julianne Martin Chotta ..... 2. Ndugu Mayagila Amram Halfani .. 3. Ndugu Mfalingundi Musa Shaabani .....	46 86 5

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
3. Makete	1. Ndugu Reuben Ramadhani Mbilinyi..... 2. Ndugu Nahum Philipo Majaliwa Ndelwa 3. Ndugu Wilson Mgambo Ntulo ..... 4. Ndugu Tuntemeko Mesaka Nnung'wa Sanga .....	10 12 82 343
4. Mufindi	1. Ndugu Joseph Saini Kwilla ..... 2. Ndugu Joseph James Mungai .....	55 444
5. Iringa Magharibi	1. Ndugu Kihwele Titus Martini ..... 2. Ndugu Kiponza Yusuf Ramadhani ..... 3. Ndugu Mgimwa William Agustao ..... 4. Ndugu Ndenga Severin Hussein ..... 5. Ndugu Kibasa Cyprian Banumutwa ..... 6. Ndugu Mdegela Kafwitengosi William ... 7. Ndugu Godson Raphael Lyamdalala ..... 8. Ndugu Lyellu Renatus Galafunga ..... 9. Ndugu Mgumba Abdallah Mussa ..... 10. Ndugu Choggia Modestus Kivatama ..... 11. Ndugu Kilangi Peter Ligungula Mahesela 12. Ndugu Luhanga James Eleuter ..... 13. Ndugu Nzelu Benedict Ildebrant .....	6 4 16 38 4 25 22 14 3 193 114 224 46
6. Njombe	1. Ndugu Makwetia Jackson Muvangila .....	615
7. Iringa Mashariki	1. Ndugu Rev. Peter Lukumbusho Mwamasika ....., 2. Ndugu Msigomba John Msangasi ..... 3. Ndugu Mlawa George Francis ..... 4. Ndugu Myalla Michael Mwandika ..... 5. Ndugu Masengo Vinance Martini ..... 6. Ndugu Salum Abdalla Islam ..... 7. Ndugu Gaifalo Yoel Mwanuke ..... 8. Ndugu Mwaluvinga Chrisspin ..... 9. Mwaduma Stephen Zachariah ..... 10. Ndugu Mpete Odo Fungameza ..... 11. Ndugu Mwasanyagi Julius Mnanike .....	445 88 85 1 2 5 31 3 29 20 2
<b>MKOA WA DAR ES SALAAM</b>		
1. Ilala	1. Ndugu Wejja Martha Michael ..... 2. Ndugu Capt. Ditopile-Mzuzuri Ukiwaona Ramadhani Mwinshiehe .....	194 92
	3. Ndugu Kyelula Kijakazi Salum ..... 4. Ndugu Watuta Sadick Mrisho ..... 5. Ndugu Sandhu Tarlochan Singh ..... 6. Ndugu Kamala Joatham Mporongoma ... 7. Ndugu Lt. Makuka Haruni Ramadhani Kondo .....	88 28 27 18 17

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jinbo la Uchaguzi</i>	<i>Waqombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
	8. Ndugu Lekamoi Eunice Veilla Ismail .....	17
	9. Ndugu Mwinyimsa Abedi Amri Saidi .....	12
	10. Ndugu Gulamali Mohamedali Gulamali .....	12
	11. Ndugu Mwinyi Juma Mwinyi .....	8
	12. Ndugu Kilawi Amani Mohamed .....	5
	13. Ndugu Likulile Mussa Ally .....	4
	14. Ndugu Mwinyigogo Zuberi Mohamed Kiliza .....	4
	15. Ndugu Mbwihiile Shabani Mohamed .....	3
	16. Ndugu Shérü Mohamed Bahadour Khan .....	3
	17. Ndugu Mabu Mumba Sosthenes .....	2
	18. Ndugu Peter Muhindi Nyamunjukya .....	1
	19. Ndugu Sombe Patrick Jacob .....	1
	20. Ndugu Mpenu Yusufu Khalfan .....	0
2. Kinondoni	1. Ndugu Hading'oka Juma Hussein .....	191
	2. Ndugu Yamungu James Charles .....	115
	3. Ndugu Che-Mponda Aleck Humphrey .....	51
	4. Ndugu Nasson Samwel Kassanga Tumbo .....	32
	5. Ndugu Kimatare Alex Moses .....	22
	6. Ndugu Dharsi Jamnadas Ramji .....	21
	7. Ndugu Komba John Damian .....	16
	8. Ndugu Mzee Issa .....	15
	9. Ndugu Msangi Ahmad Hamis Mohamed .....	14
	10. Ndugu Sozigwa Daniel Andrea .....	9
	11. Ndugu Lengalenga Laurence Gabriel Haule .....	8
	12. Ndugu Rahman Mohamed Kibugila .....	8
	13. Ndugu Mwakipunda Nsubisi Samuel .....	7
	14. Ndugu Wilambile Lukikó Some .....	6
	15. Ndugu Mwakatobe Ayub Paul S. E. ....	6
	16. Ndugu Vitus Lyamkuyu George .....	5
	17. Ndugu Semondo Ahmed Mwinjuma .....	2
	18. Ndugu Hamza Tatu Saidi .....	2
	19. Ndugu Sadallah Radhid Mohamed Omari .....	2
	20. Ndugu Mmanga Suleiman Mmanga .....	2
	21. Ndugu Gibson Andrew Nyambele .....	2
	22. Ndugu Kiremera Furaha Hassan .....	1
	23. Ndugu Maswi Megewa Samwel .....	1
	24. Ndugu Mwihumbo Gaspar Mkodombo .....	1
	25. Ndugu Maingo Shadrack Nfereja .....	0
	26. Ndugu Bongo Ally Mohamed .....	0
	27. Ndugu Jazza Salim Almasi Seif .....	0
	28. Ndugu Honero Ferdinand Setumbi .....	0
	29. Ndugu William Panne Jacob Mkweche .....	0
	30. Ndugu Mchuzi Samaka Buido Katengo .....	0
	31. Ndugu Dilunga Milkion Michael .....	0
	32. Ndugu Elia Michael Pandisha .....	0
	33. Ndugu Dibwe Omari Said .....	0

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
3. Temeke:		
	1. Ndugu John Lesta Lyanakile .....	92
	2. Ndugu Hamisi Omari Tajiri .....	68
	3. Ndugu Baina Kasim Saidi .....	7
	4. Ndugu Nyakuyeya Julius Makoye .....	10
	5. Ndugu Kajembe Frank Semagongo .....	29
	6. Ndugu Mwakyanjala Patrick Eliakim .....	10
	7. Ndugu Ramadhani Saidi Somboko .....	10
	8. Ndugu Goloka Omari Masoud .....	12
	9. Ndugu Haule Jacob Titus .....	0
	10. Ndugu Mshenene Innocent Chagu .....	19
	11. Ndugu Kalambo Patrick Martin .....	16
	12. Ndugu Hozza Mathey Sabuni .....	37
	13. Ndugu Kilungi Saidi Mohamed .....	8
	14. Ndugu Lunda Leonard Joatham .....	2
	15. Ndugu Magomba Swalehe Masoud .....	3
	16. Ndugu Mbaruku Pongwe Balozi .....	28
	17. Ndugu Masudi Alli Masudi .....	50
	18. Ndugu Harith Mahmoud Hamduni .....	6
	19. Ndugu Swalehe Kapuli Migetto .....	12
	20. Ndugu Melkiory Vicent Ngonyani .....	10
	21. Ndugu Kuruthumu Abdallah Ally .....	12
	22. Ndugu Daniel Peter Mkoma Kipugulu ....	3
	23. Ndugu Ahemed Salim Mwerani .....	34
	24. Ndugu Ndimi Conrad Ngaliwinglo .....	0
	25. Ndugu Mayagilo Justin Doto .....	9
	26. Ndugu Kamba Mohamed Salum .....	19
	27. Ndugu Bushiri Juma Kilungo .....	84
	28. Ndugu Shengena Timothy Michael .....	1
	29. Ndugu Museveni Portian Canisio .....	3
	30. Ndugu Chubi Omar Saidi Lungungu .....	9
	31. Ndugu Msakandeo Mohamed Maneno ....	1

**MKOYA WA DODOMA**

1. Bahi		
	1. Ndugu Zakaria D. Mboma .....	7
	2. Ndugu Yared E. Mabalwe .....	5
	3. Ndugu Wilson K. Gombo .....	52
	4. Ndugu Salen N. Mhilu .....	7
	5. Ndugu Francis M. Chakoo .....	43
	6. Ndugu Bernatdin L. Mwaja .....	21
	7. Ndugu Saïd A. Chilatu .....	8
	8. Ndugu Mtawa J. Mtawa .....	9
	9. Ndugu Simon M. Mwang'ata .....	105
	10. Ndugu Peter R. Mwimbwa .....	168
	11. Ndugu Masiita Godwin Masiita .....	10
	12. Ndugu Nyambuya Mwaluko Mkozi .....	10
	13. Ndugu Barnabas Tirjothy Msambili .....	3
	14. Ndugu Jalla Richard Chibada .....	9
	15. Ndugu Leonard Luhamba Mwaluko .....	7

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
	16. Ndugu Mhugu Emillian Mganga .....	6
	17. Ndugu Chilongozi Amandus Adam .....	7
	18. Ndugu William Jonathan Kusila .....	59
	19. Ndugu Mahugu Thadei Hoya .....	13
2. Chilonwa	1. Ndugu John Malecela .....	379
	2. Ndugu Yohana M. Mazengo .....	114
	3. Ndugu Reuben N. Shosho .....	26
	4. Ndugu Denis W. Bendera .....	33
3. Dodoma Mjini	1. Ndugu Stanley Godfrey Mbogoni .....	4
	2. Ndugu Hosea Francis Daniel Sahali .....	7
	3. Ndugu Salehe Ramadhani Simba .....	2
	4. Ndugu Capt. Khery Kissinger Hassani .....	3
	5. Ndugu Severini Andrea Supa .....	120
	6. Ndugu John Gpanha Mathew Mgogolo .....	0
	7. Ndugu Maurice Margeson Nchimbi Mwandikaulaya .....	2
	8. Ndugu Sara Joy Mwenge .....	45
	9. Ndugu Benjamin Zebedayo Mazengo .....	2
	10. Ndugu Benedict Rajabu Msuya .....	10
	11. Ndugu Donald Mazengo Kusenba .....	81
	12. Ndugu Lt. Bernard Frederick Sule .....	3
	13. Ndugu Ally Rajabu Mkamba Suleiman .....	7
4. Kondoa	1. Ndugu Mustafa Selemani Nyang'anyi .....	674
5. Kongwa	2. Ndugu Leonard Candid Mujungu .....	56
	1. Ndugu Chibwayea Isaiha Lenjmet .....	45
	2. Ndugu Mwingwa Pearson Msangu .....	56
	3. Ndugu Helena Margaret Jumbe .....	48
	4. Ndugu Chamwela Sylvester Jafet .....	22
	5. Ndugu Machitte Jackson Samila .....	15
	6. Ndugu Mbogo Yakobo Daniel .....	9
	7. Ndugu Lusingo Ezri Esrom .....	8
	8. Ndugu Mzuli Moses George .....	2
	9. Ndugu Chibanhila Joshua Malaki .....	81
	10. Ndugu Senyagwa Gideon Ayubu Lemunje .....	215
6. Mpwapwa	1. Ndugu Sindamwaka Michael Maganza .....	103
	2. Ndugu Mazanda Francis Barnett .....	28
	3. Ndugu Harold Gamalsel Lewjima .....	42
	4. Ndugu Ngoitamile Gabriel Laurent .....	25
	5. Ndugu Mwiki Geoffrey Sidiadi .....	22
	6. Ndugu Dickson Lameck Mugongo .....	18
	7. Ndugu Msoloka Yohana Elisha .....	5
	8. Ndugu Lubeleje George Malima .....	115
	9. Ndugu Mtaki Ali Saidi .....	148
7. Ntomoko	1. Ndugu Sogora Ismail Matumbwi .....	11
	2. Ndugu Muyombo Shabani Selemani .....	470
	3. Ndugu Affa Gabriel Paschal .....	10

**NYONGEZA "B" (inaendelea)**

<i>Jimbo la Uchaguzi</i>	<i>Wagombea</i>	<i>Idadi ya Kura</i>
	4. Ndugu Saida Juma Gamu .....	70
	5. Ndugu Wenga Lucas Gele .....	4
	6. Ndugu Degera Paschal Constantine .....	51
	7. Ndugu Niwanga Theonas Gabriel .....	9
	8. Ndugu Lt. Budeka Hussein Hinte .....	49
	9. Ndugu Idrisa Mohamed Noti .....	15
	10. Ndugu Mafita James Alois .....	7
	11. Ndugu kadukadu Ramadhani Abdallah ...	19
	<b>MKOA WA KAGERA</b>	
1. Bukoba Vijijini	1. Ndugu Rwegasira Emmanuel William ....	330
	2. Ndugu Rutageruka Novati Sumeon .....	310
	3. Ndugu Rutaraka Bitakwese Emmanuel ...	124
	4. Ndugu Kymaukumu II, Serapion Lwamjongo .....	39
	5. Ndugu Lt. Mukandara Doderick Gaspar .	29
	6. Ndugu Kamugisha Laurent .....	24
	7. Ndugu Mutayabarwa, Sililo Mweyunge ...	13
	8. Ndugu Kyaruzi, Augustion Rwenabura ...	6
	9. Ndugu Namba Francis Mkella .....	5
	10. Ndugu Capt. Kalokola Badru Nuru .....	3
	11. Ndugu Rwebangira Joseph Mtakangwa ...	2
2. Karagwe	1. Ndugu Byetima John Eliakim .....	157
	2. Ndugu Rwechungura Salvatory Tirukaizile	147
	3. Ndugu Kalokola Muzzamil Mussa .....	58
	4. Ndugu Raphael Kinyima Gahoile .....	38
	5. Ndugu Nshobeirwe Christian Ihahuza ....	11
	6. Ndugu Justus kamuhabawa Ndyanabo ....	4
3. Bukoba Mjini	1. Ndugu Luangisa Samwel Mtambala .....	116
	2. Ndugu Katarala Mujuni Joseph .....	58
